**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU NACHINGWEA**

Simu : 0732933334
Fax : 0732933334
E mail:**nachingweatc@gmail.com**
au ***nachingweatc@moe.go.tz***
***Website: www.nachingweatc.ac.tz***

S. L. P. 39,
**Nachingwea**.
24.06.2026

Unapojibu tafadhali nakili:
**Kumb: Na. NCCU/A.3/6/36**
Ndugu, ……………………………………..

……………………………………..

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI KWA LUGHA YA KIINGEREZA KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

**1. UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya **Stashahada ya Elimu ya Ualimu wa Awali kwa lugha ya Kiingereza (Miaka 2)**/ ***Stashahada ya Elimu ya Ualimu wa Awali kwa lugha ya Kiingereza kwa njia ya Masafa (Miaka 3-4)*** katika chuo cha Ualimu Nachingwea kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

Mwelekeo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutokana na maboresho ya Sera mpya ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023 ni kumuandaa mwalimu mahiri na mwenye ujuzi stahiki katika Ualimu Elimu ya Awali. Aidha, mafunzo utakayopata yatakupatia sifa na ujuzi wa kufundisha hapa nchini na nje ya nchi kwa kuzingatia fursa za soko la ajira ndani na nje ya nchi.

**2. MAHALI CHUO KILIPO.**

Chuo kipo katika Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Nachingwea, kwa wanaotoka mikoani kupitia Dar es Salaam mabasi yanapatikana stendi ya Temeke Mwisho na Mbagala Rangitatu. Kwa wanaotoka mikoa mingine kupitia njia ya Songea panda magari ya masasi, Mtwara au Dar es salaam na shuka stendi ya Masasi mjini kisha panda magari yanayoenda Nachingwea mjini. Ukifika Nachingwea mjini chuo kipo umbali wa kilometa moja kutoka stendi kuu ya mabasi. Ukifika unaweza kutumia usafiri wa pikipiki au bajaji kwa gharama ya Tsh.2000 kwa pikipiki na Tsh. 3000 kwa bajaji.

**3. MAFUNZO:**

Mafunzo haya ni ya muda wa miaka miwili isipokuwa kwa wanachuo watakaosoma kwa njia ya masafa, watapaswa kukamilisha mafunzo katika muda wa Miaka 3-4. Mafunzo yanajumuisha mafunzo ya nadharia chuoni na vitendo katika mazingira halisi ya Shule

za Awali na Msingi ambapo mafunzo kwa vitendo yatafanyika kulingana na utaratibu wa Chuo na maelekezo ya Wizara.

## 4. KURIPOTI CHUONI

Unapaswa kuripoti chuoni ndani ya siku 14 kuanzia tarehe 17/08/2026. Utahitajika kuhudhuria mafunzo kabilishi (Orientation Course) yatakayoanza mara moja. Mafunzo hayo ni maalumu ili kukuwezesha kuishi na kujifunza vema katika kipindi chote utakachokuwepo chuoni.

***NB: Wanachuo wa Stashahada ya Elimu ya Ualimu wa Awali kwa lugha ya Kiingereza kwa njia ya Masafa watapewa taarifa kuhusu kituo na tarehe ya kuanza mafunzo kabilishi.***

## 5. TARATIBU ZA USAJILI

Ili usajiliwe, utapaswa uwe na vitu vifuatavyo:-

(i) Barua ya kuitwa kujiunga na Chuo (joining instructions form).

(ii) Cheti halisi cha kumaliza kidato cha Nne/Sita (Certificate of Secondary Education Examination/Advanced Certificate of Secondary School Examination) pamoja na ‘School Leaving Certificate-Original

(iii) Cheti halisi cha kuhitimu Mafunzo ya Ualimu Daraja IIIA (Grade A Teachers Certificate Examination -GATCE) au Result Slip kwa wale waliomaliza kidato cha sita/Ualimu mwaka 2026.

(iv) Cheti halisi cha kuzaliwa- (Original Birth Certificate).

(v) Walimu kazini, pamoja na maagizo ya hapo juu (i-iii) wanapaswa kuja na barua ya ruhusa ya kwenda masomoni kutoka kwa mwajiri wake.

(vi) Pamoja nakuja na vyeti halisi ni lazima uje na nakala (fotokopi) za vyeti vyote kwa ajili ya kuweka kwenye faili la kumbukumbu binafsi. Mwanachuo atakayekuja na nakala za vyeti bila vyeti halisi hatapokelewa.

(vii) Fomu ya daktari/medical examination form, ijazwe na daktari wa Hospitali ya Serikali.

(viii) Picha 2 za rangi (passport size).

(ix) Kulipa ada na michango ni kigezo muhimu cha kukamilisha usajili.

**Tahadhari:** Chuo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kina uwezo wa kubaini wale wote wanaotumia vyeti visivyo vyao au ambavyo siyo halali na watakaobainika watafikishwa mbele ya vyombo vya sheria kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

## 6. ADA NA MICHANGO MBALIMBALI

**Mahitaji ya ada na michango ni kama ifuatavyo:-**

(a) **Ada/Karo ya Chuo: (Kwa wanachuo wote ikiwa ni pamoja na wale wa Mafunzo kwa njia ya Masafa)** Ada ya mafunzo kwa mwaka ni Shilingi **450,000/=** Ada hii

inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili (Shilingi **225,000/= kwa kila muhula)** katika mwaka wa mafunzo. Ada inaweza kulipwa baada ya kufika chuoni au ukiwa nyumbani baada ya kufanya mawasiliano na **mhasibu (0785 551 600)** atakayekupa 'control number" ya malipo ya maduhuli ya serikali kwa njia ya Kielektroniki (GePG). "Control number" hiyo unaweza kulipia kupitia benki yoyote au wakala wa benki au kupitia mitandao ya simu. (***Kumbuka kutunza 'pay in slip' ya malipo ya benki au ujumbe wa miamala ya malipo kupitia mitandao ya simu).***

Kwa mawasiliano zaidi waweza kupiga simu **0785 551 600 (Mhasibu) na Msajili ni 0713 509 205**. Chuo hakipokei fedha taslimu, hivyo fedha zote zilipwe kupitia benki. (***Hairuhusiwi kulipa fedha taslimu kwa mhasibu)***.

**(b)** Michango ilipwe kwa akaunti namba **70403500039,** Jina la akaunti ni **COLLEGE FUND ACCOUNT NACHINGWEA Benki ya NMB. Hakikisha unatunza na kuwasilisha hati ya malipo (pay in slip) kwa mhasibu wa chuo**. Tunza vizuri stakabadhi utakazopewa na mhasibu chuoni ili uzitumie kuthibitisha kukamilisha michango uliyotoa zitakapohitajika. **Kamilisha mahitaji hayo bila kukosa. Hautapokelewa na kusajiliwa endapo hutakamilisha mahitaji hayo.** Michango hiyo ni kama ifuatavyo:

- Serikali ya Wanachuo Tshs. 5,000/= kwa mwaka;
- Afya,Usafi na Mazingira Tshs 20,000/= kwa mwaka;
- Usajili na Kitambulisho Tshs. 20,000/=kwa mwaka;
- Michezo Tshs. 30,000/= kwa mwaka;
- Ulinzi Tshs. 30,000/= kwa mwaka;
- Vibarua Tsh 20,000/= kwa mwaka;
- Ukarabati Tshs. 25,000/= kwa mwaka;
- Rimu 1 ya karatasi A4 kwa mwaka;
- Jembe likiwa na mpini wake;
- Wanaume: Kifaa kimojawapo kati ya ***hard bloom au Reki.***
- *Wanawake: Kifaa kimojawapo kati ya* ***soft bloom au squeezer.***

**Mengineyo Muhimu (Kwa wanachuo wa kozi ya miaka miwili):**

- Mahafali tsh 15,000/=kwa mwaka.
- Uje na godoro ft $2^1/2$ kwa 6 ft **aidha Chuo kina magodoro machache na kinakodisha godoro kwa Tsh. 10,000/= kwa muhula**
- Mchango wa **Tsh. 50400/= kwa mwaka kwa ajili ya BIMA ya afya.**
- **Ada ya mitihani ya Taifa (NECTA) 50,000/= (Kwa mwaka wa II)**

**Michango kwa Stashahada ya Elimu ya Ualimu wa Awali (Kwa Lugha ya Kiingereza) kwa Njia ya Masafa.**

**a)** Huduma ya kwanza (matibabu) Tshs. **10,000/=** kwa mwaka.
**b)** Usajili na kitambulisho Tshs**. 20,000/=** kwa mwaka.
**c)** Serikali ya WanachuoTshs. **5,000/=** kwa mwaka.

**d)** Ukarabati Tshs. **25,000/=** (kwa mwaka).
**e)** Elimu ya Michezo Tshs. **30,000/=** kwa mwaka.
**f)** Usafi na utunzaji mazingira **20,000/=** kwa mwaka.
**g)** Ufuatiliaji na Uendeshaji wa Mafunzo Tsh. 40,000/= kwa mwaka.

**Jumla ya michango inayotakiwa kulipwa ni Tshs. 150,000.00 kwa mwaka.**

**Muhimu:**

(i) ***Fedha za michango*** zilipwe benki ya ***NMB Akaunti Namba*** **70403500039,** Jina la akaunti ni **COLLEGE FUND ACCOUNT NACHINGWEA**

(ii) Tunza hati halisi ya malipo ya benki (original pay slip) ikionesha kiasi kilicholipwa na yenye jina kamili la mwanachuo au ujumbe wa Malipo kwa mitandao ya simu.

(iii) ***Usichanganye malipo ya ada na michango kwenye akaunti moja.***

(iv) Hakikisha unakuwa na Bima ya Afya.


(v) Ada ya Mitihani ya Taifa (NECTA) TSh. 50,000/= itatolewa mwaka wa mwisho wa Mafunzo.

## 7. MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA

- Madaftari makubwa ya kutosha (angalau 12)
- Majalada matupu (flat files) kwa ajili ya mkoba wa kazi (Portifolio) kwa kila somo.
- Muhutasari wa Elimu ya Awali kwa Lugha ya Kiingereza.
- Mathematical set- Mkebe wa Hisabati.
- Simu janja/Kishikwambi/Kompyuta inayoweza kuunganishwa na mtandao wa intaneti (**Kwa wanachuo wa Njia ya Masafa)**
- Bando la Maunganisho ya mtandao (**Kwa wanachuo wa Njia ya Masafa**).

## 8. MAVAZI

**Sare ya Wavulana:** Suruali ya kushona iwe ya rangi ya **“Dark Blue”** yenye mifuko pembeni mfuko mmoja wa nyuma, na rinda mbili kila upande (isiyobana). Shati bluu bahari (light blue) la mikono mirefu na lisilobana na tai ya dark blue. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika na soksi nyeusi. Uje na nguo za michezo (bukta, jezi ya bluu (T-shirt na kaptula), **Track suit** za rangi ya **Bluu** na raba za rangi yoyote isiyo nyeupe). Vilevile sweta la rangi ya blue nyeusi (Dark Blue) pamoja na koti la rangi ya ‘Dark Blue’ litakalofanana na rangi ya Suruali. Muonekano wa suruali unaotakiwa ni kama ifuatavyo:



**Sare ya Wasichana:** Sketi yenye mshono wa vi (V) ya rangi ya "**Dark Blue**" inayovuka magoti kwenda chini, shati bluu bahari **(light blue**) la mikono mirefu (lisilobana) na tai ya rangi ya "**dark blue**", viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye visigino vifupi na soksi nyeusi. Uje na nguo za michezo (jezi ya bluu, track suit za rangi ya **Bluu** na raba za rangi yoyote isiyo nyeupe) na sweta la rangi ya Bluu nyeusi **(Dark blue**). Muonekano wa sketi unatakiwa kuwa kama ifuatavyo:



**NB:** Wanachuo wa kike madhehebu ya Kiislamu wanaruhusiwa kuvaa sare ndefu za chuo na"hijab" ya kitambaa cha bluu bahari.

9. **DINI na SIASA:**
Chuo kama taasisi ya serikali hakina dini wala chama cha siasa. Hata hivyo, unaruhusiwa kuabudu kwa imani yako na kushiriki katika masuala ya kisiasa bila kuathiri ratiba, taratibu na kanuni za chuo. Hakikisha imani yako au ushiriki wako wa masuala ya kisiasa hauathiri taratibu za chuo wala kuvunja amani. Siasa/misimamo mikali ya dini havina nafasi hapa chuoni. Masuala ya dini/siasa kamwe hayapaswi kuathiri taratibu za uendeshaji wa chuo.

10. **VIFAA VYA MALAZI, USAFI NA CHAKULA:**
Unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako binafsi – pazia moja kwa ajili ya chumba chako lenye ukubwa wa sm 140 kwa sm 90, ndoo na vyombo vya kulia chakula. Pia uje na mashuka mawili au Zaidi ya kulalia ya rangi yoyote, chandarua na mto. Vifaa hivi vilivyotajwa vinapatikana pia hapa Nachingwea mjini kwenye maduka, hivyo waweza kuamua kuja na fedha na kuvinunua huku ili kupunguza usumbufu na gharama za kuvisafirisha.

Kauli mbiu ya chuo ni "**Nitajielimisha**"

"**Ni Tunu kuwepo katika Chuo hiki, kitunze kiwe safi mara zote**". Itumie vizuri Tunu hiyo ili kupata maarifa na stadi bora kujenga mwelekeo unaokubalika katika Taaluma ya Ualimu.

**TUNAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA YA KUJA CHUONI**
**KARIBU CHUO CHA UALIMU NACHINGWEA**

**…………………………………..**
**Justine L. Ngimba**
**Mkuu wa Chuo**

**THE GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

To: Medical Officer
……………………………………….
………………………………………….
………………………………………….

From: Principal,
Nachingwea Teachers' College
P.O.Box 39,
NACHINGWEA.

Mr./Mrs./miss ........................................................................................... (Name in full)

Please examine the above as to is/her physical and mental fitness for a fulltime teacher training course. The examination should include the following categories (I – ii) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case a defend. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate in eligible for the course.

(a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal disease
(f) Other serious diseases
(g) Leprosy Speech
(h) Neurosis
(i) Pregnancy
(j) Epilepsy
(k) Mental and Physical fitness

...............................................
Principal

……………………………………………………………………………………………………

**PART B:** (To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that he/ she is physical fit/ unfit and mentally fit/ unfit for a fulltime teacher course.

I. (a) Eye – sight……………………………………………………………………………..

(b) Hearing …………………………………………………………………………………

(c) Limbs ……………………………………………………………………………………

(d) Speech …………………………………………………………………………………

(e) Venereal disease ………………………………………………………………………

f) Leprosy…………………………………………………………………………………..

(g) Epilepsy ...........................................................................................................

(h) Neurosis ………………………………………………………………………………..

(i) Other serious diseases……………………………………………………………………..

(j) Pregnancy…………………………………………………………………………………

(k) Mental and physical fitness ……………………………………………………........

Date ………………………………………..Signature ………………………………..……